

HALMASHAURI YA MJI WA MAKAMBAKO

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE
03/11/2021**

WAJUMBE WALIOHUDHURIA

NA.	JINA LA MJUMBE	WADHIFA
1.	Bw. Eliud Mwakibombaki	Mwenyekiti
2.	Bi. Eunice Komba	Katibu
3.	Dr. Alexander Mchome	Mjumbe
4.	Bi. Norbetha Nyoni	Mjumbe
5.	Bi. Zuena Ungele	Mjumbe

WAJUMBE WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA

1.	Bi. Appia Mayemba	Mjumbe
----	-------------------	--------

SEKRETARIETI.

NA	JINA	WADHIFA
1.	Bi. Melania Siame	Afisa Manunuzi
2.	Bw. Barnabas Slaqwara	Afisa Ugavi

AGENDA ZA KIKAO

Kufungua Kikao:

1. Kufungua Kikao
2. Kupokea taarifa ya kuanza mchakato wa ujenzi wa miradi ya UVIKO – 19.
3. Kufunga kikao.

AGENDA NAMBA 01/11/2021 KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao **saa 5:15 mchana** akiwakaribisha wajumbe kwenye kikao na kuwaomba kujadili agenda zilizoko mezani.

AGENDA NAMBA 02/11/2021 KUPOKEA TAARIFA YA KUANZA MCHAKATO WA UJENZI WA MIRADI YA UVIKO – 19.

Mwenyekiti alisoma taarifa ya kuanza mchakato wa miradi ya UVIKO – 19, aliwaeleza wajumbe wa Bodi ya Zabuni kuwa Halmashauri imepokea fedha kiasi cha Shilingi za

KItanzania **1,140,000,000.00** katika mchanganuo ufuatao:- Kiasi cha **Tzs. 520,000,000.00** kwa ajiri ya ujenzi wa madarasa 26 ya sekondari kila chumba cha darasa kwa gharama ya **Tzs. 20,000,000.00**, **Tshs 240,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa shule shikizi 5 na sekondari 1 zeny vyumba nya madarasa 12 kila moja. **Tzs.80,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Bweni wenye mahitaji maalumu, aidha mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa kiasi cha **Tzs.300,000,000.00** kimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa jingo la dharura na kiasi **Tzs.90,000,000.00** kimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi tatu kwa moja.

Wajumbe waliipokea taarifa na kuipongeza serikali kwa kuleta fedha.

MAAMUZI


Wajumbe kwa pamoja walijadiliana nakukubaliana kuwa taratibu za manunuzi zianze kufanyika kwa kutumia njia ya force akaunti kama mwongozo ulioletwa na TAMISEMI unavyoelekeza, aidha wajumbe walielekeza fedha hizo zipelekwe maeneo husika na kuanza mchakato mara moja.

AGENDA NAMBA 03/11/2021 KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti alifunga Kikao mnamo saa 06:20 mchana kwa kuwashukuru wajumbe kwa mahudhilio na mchango wa mawazo.


UMETHIBITISHWA

Mwenyekiti

Saini


Tarehe 17/12/2021

Katibu

Saini .....

Tarehe 17/12/2021